# UJE ROHO MTAKATIFU

Magere E. Nwasya
Mwadui
Shinyanga







2.Uje baba wa maskini
Uje mtoa vipaji
uje mwanga wa mi-oyo/..

3.Ee mfariji mwema sana
ee rafiki mwa-nana
Ewe raha mu-starehe

4.Kwenye kazi u pumziko
kwenye joto burudiko
umfutaji wa-machozi.

5.Ewe mwanga wenye heri
uwajaze waamini
neema yako mi-oyoni.

6.Bila nguvu yako wewe
mwanadamu hana kitu
kwake yote yanakosa.

7Osha machafuko yetu
panyeshee pakave petu
na kuponya- ma-jeraha..

8.Ulegeze ukaidi
pasha moto ubaridi
nyosha upotevu wote.

9.wape waamini wako
wenye tumaini kwako
paji zako-zote saba.

10.Wape tozo ya fadhila
wape mwisho bila hila
wape heri ya mi-lele.

11.A-mina aleluya
A-mina aleluya
a-mina aleluya.

Copied by Sitta Af